

# Maadhimisho ya Maombi Duniani kote—2024

**Sifa**—Mungu ni mwema; mkuu, mkuu juu ya vyote, ni mkuu zaidi ya tabia na ubora; ni wa ajabu katika ukubwa wake, Mwenye ukuu, mamlaka, nguvu na hapimiki.

Ee Bwana, ukuu ni wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni vyako; ufalme ni wako, Ee BWANA, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote. 1 Nyakati 29:11 SUV

Ee BWANA Mungu, umeanza kumwonyesha mtumishi wako ukubwa wako, na mkono wako wa nguvu; kwani kuna Mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu? Kumbukumbu la torati 3:24 SUV

BWANA ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana, Wala ukuu wake hautambulikani. Zabri 145:3 SUV

Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho. Efeso 1:18-20 SUV

**Toba**—Ee Mungu, unirehemu, Sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, Uyafute makosa yangu. Zaburi 51:1 SUV

**Shukrani**—Kwa ajili ya neno lako, na kwa moyo wako mwenyewe, umetenda makuu hayo yote, ili umjulishe mtumwa wako. Kwa hiyo, wewe ndiwe kuu, Ee BWANA Mungu, kwa maana hakuna kama wewe, wala hapana Mungu mwingine ila wewe, kwa kadiri tulivyosikia kwa masikio yetu. 2 Samueli 7:21-22 SUV

## Maombezi:

### Watoto wetu

Mungu naomba \_\_\_\_\_ asimame imara, awe na nguvu ya Mungu na Naiombea nafsi ya \_\_\_\_\_ na vyote anavyoviomba kwa utukufu wa Mungu! Naomba kizazi cha \_\_\_\_\_ Wamtukuze na Kumpa sifa Bwana Mungu na Nguvu zake pamoja na matendo ya ajabu aliyoyafanya. (Zab 138:3, Luk 1:46, Zab 78:4b)

### Kwa waliopotoka

Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Warumi 10:9 SUV

### Wanafunzi

Lakini akawaokoa kwa ajili ya jina lake, Ayadhihirishe matendo yake makuu. Zaburi 106:8 SUV

### Walimu

Utajiri na heshima hutoka kwako wewe, nawe watawala juu ya vyote; na mkononi mwako mna kuwatukuza na kuwawezesha wote. 1 Nyakati 29:12 SUV

### Shule

Nami nitajitukuza, na kujitakasa, na kujidhihirisha, mbele ya macho ya mataifa mengi; nao watajua ya kuwa mimi ndimi BWANA. Ezeieli 38:23 SUV

### Huduma ya Wamama Waombaji.

BWANA ni mwema kwa watu wote, Na rehema zake zi juu ya kazi zake zote. Zaburi 145:9-12 SUV



Wamama Waombezi Kimataifa